

Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa Kwa Magari Matano Kwa Ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki Kwa Kampuni ya East African Crude Oil Pipeline Limited

TANGAZO LA SERIKALI NA. 325 la tarehe 26/4/2024

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA
(SURA YA 147)

—
AMRI
—

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MATANO KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI KWA KAMPUNI YA EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE LIMITED YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Matano kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kwa Kampuni ya East African Crude Oil Pipeline Limited ya mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika kuanzia tarehe 6 Machi, 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa Magari Matano yaliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii, zilizoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha na Kampuni ya East African Crude Oil Pipeline Limited kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki unasamehewa.

Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa Kwa Magari Matano Kwa Ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki Kwa Kampuni ya East African Crude Oil Pipeline Limited

Tangazo La Serikali Na. 326 (Linaendelea)

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa Magari hayo yatatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yaliyotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo tarehe 5 Septemba 2024.

JEDWALI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

Na.	Aina	Chassis Na.	Injini Na.
1.	Ford Everset XLT 2.0 Bi- Turbo, 4x4	6FPRXXMAWRPU70891	YNWQRPU70891
2.	Ford Everset XLT 2.0 Bi- Turbo, 4x4	6FPRXXMAWRPU70892	YNWQRPU70892
3.	Ford Everset XLT 2.0 Bi- Turbo, 4x4	6FPRXXMAWRPU70893	YNWQRPU70893
4.	Ford Everset XLT 2.0 Bi- Turbo, 4x4	6FPRXXMAWRPU70894	YNWQRPU70894
5.	Ford Everset XLT 2.0 Bi- Turbo, 4x4	6FPRXXMAWRPU72988	YNWQRPU72988

Dodom

4 Aprili, 2024.

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU

Waziri wa Fedha